



UPOKEZI WA HADITHI FUPI KWA WANAFUNZI

Na

Raphael Khanyaka Oduori

Shule ya Sayansi za Kijamii

(Idara ya Lugha)

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya Shahada ya Uzamili (Master of Arts) katika Chuo Kikuu cha Mount Kenya.

FEBRUARI, 2014

IKISIRI

Utafiti huu umeshughulikia Upokezi/Mwitikio wa Wanafunzi wa shule zetu za upili nchini Kenya wanaposoma Hadithi Fupi. Somo la Fasihi, kwa ujumla, ni pana mno. Utanzu wa Hadithi Fupi ni fani mpya katika mtaala wa shule za upili nchini Kenya. Diwani ya kwanza yenye mkusanyiko wa hadithi fupi ilikuwa *Mayai Waziri wa Maradhi* (K. W. Wamitila - Mhariri). Ilianza kutahiniwa katika mtihani wa KCSE kwanzia mwaka wa 2006 hadi mwaka 2012. Baada yake, diwani ya pili ikateuliwa; hii ni *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (Ken Walibora na Said A. Mohamed - Wahariri). Maadam hakuna utafiti ambao umekwishafanywa kutathmini upokezi wa utanzu wa Hadithi Fupi katika shule zetu za upili huenda maswali wanayoulizwa katika mtihani yanawakanganya wanafunzi hawa au wanatoa majibu yanayoonyesha tofauti tofauti – lakini yenye mashiko - kwa swali moja. Utafiti umefafanua kuwa kila mwanafunzi, kivyake, hupokea kila hadithi kwa namna yake, jambo ambalo huenda likawa kinyume na maelekezo na matarajio ya walimu na wahakiki wengine. Utafiti uliongozwa na nadharia ya Upokeaji wa Fasihi/Mwitikio wa Msomaji. Waasisi na watetezi wake wakuu ni Stanley Fish (1980), Jane Tompkins (1980) na Wolfgang Iser (1974, 1978). Inanua kubainisha na kufafanua kadhaa zinazomkutanisha msomaji na kazi za fasihi. Inaamini kuwa kila kazi ya fasihi ina maana kufuatana na msomaji binafsi na jinsi anavyoichukulia. Kuwa kila kazi ya fasihi huwa na maana ya kipekee kwa kila msomaji binafsi kutokana na tajiriba yake ya zamani. Kuwa msomaji ni kiungo muhimu katika ufasiri wa tungo. Kuwa hujenga “maana” yake kutokana na “mtagusano” kati yake na kazi anayosoma, pamoja na mtazamo na tajiriba yake maishani. Kwa kuwa msomaji hubeba filosofia yake, tajiriba yake na kiwango chake cha elimu, ufasiri wa kila mmoja huwa wa kipekee na wa kibinafsi. Ni utafiti ambao uliegemea maktabani na nyanjani. Maktabani ulinufaika kwa udurusu wa vitabu, miswada, majarida, makala na tasnifu mbali mbali zinazoangazia swala la nadharia ya Upokezi/Mwitikio wa Msomaji, mbali na kusoma diwani ya *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine*, huko nyanjani ukijikita katika wilaya ya Trans – Nzoia Magharibi, Kaunti ya Trans – Nzoia, ambapo mtafiti aliteua sampuli ya makusudi iliyojumuisha shule nane za viwango tofauti tofauti, ambapo wanafunzi walitarajiwa kutoa upokezi wao wa dhana ‘Mwendawazimu’ kwa kuangazia hadithi teule kutoka kwa diwani ya *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine*. Matokeo ya utafiti huo ni johari kwa walimu na wakuza-mitaala katika juhudi zao za kuneemesha na kustawisha utanzu wa Hadithi Fupi. Aidha, utawaelekeza kuwatungia wanafunzi hawa maswali ambayo yatatilia maanani ukweli kuwa kila mwanafunzi huwa na fasiri yake ya kipekee kuhusu kila hadithi, hivyo basi kuepukana na maswali yanayolenga tu mwelekeo fulani, au yenye miongozo inayotilia maanani fasiri na mielekeo yao. Matokeo ya utafiti huo yametolewa kwa njia ya kimaalezo katika sura tano.